# UJIRANI Mwema

ISO 9001:2015 Certified

HIFADHI NA JAMII

Januari - Machi 2023



Ukurasa **6** WATOA MAENEO YAO BURE KUPISHA BARABARA HIFADHI YA TAIFA MTO UGALLA

Ukurasa **26** TANAPA YAIPAISHA SHULE KIGOMA, KUPANDISHWA HADHI

# Ilani ya Arusha



*"Uhai wa wanyamapori wetu ni jambo la muhimu sana kwetu sisi sote Afrika. Hawa viumbe-pori pamoja na mazingira-pori wanayoishi si tu ni muhimu kwa sababu ni chanzo cha maajabu na kuvutia bali hivi ni vitu muhimu katika rasilimali zetu za asili na kwa mustakhabali wa maisha yetu na ustawi wetu.*

*Katika kukubali udhamini wa wanyamapori wetu, tunatangaza kwa dhati kwamba tutafanya kila kitu kilicho ndani ya uwezo wetu ili kuhakikisha kwamba vitukuu vinaufurahia utajiri na urithi huu wenye thamani kubwa.*

*Uhifadhi wa wanyamapori na maeneo yenye mapori unahitaji maarifa ya kitaalamu, nguvu kazi yenye mafunzo, na fedha, na tunatarajia maTaifa mengine kushirikiana pamoja nasi katika kazi hii muhimu - ambayo mafaniko yake au kushindwa kwake si tu kwamba kunaliathiri bara la Afrika bali dunia nzima"*

**Mwalimu Julius K. Nyerere,**
Septemba, 1961 Arusha

**Bodi ya Uhariri**


**Mhariri Mkuu:**
William S. Mwakilema

**Mhariri Mwandamizi:**
Dkt. Bakari Mnaya

**Wahariri Wasaidizi:**
Catherine Mbena
Samwel Nassari

**Wahariri Washauri:**
Claud Gwandu
Patience Magubira

**Wasanifu wa Kurasa:**
Kitengo cha Uchapishaji - TANAPA




UJIRANI MWEMA
ni jarida linalotolewa na
Hifadhi za Taifa Tanzania
Kitengo cha Uhifadhi Mahusiano ya Jamii, TANAPA Makao Makuu,
Barabara ya Dodoma,
S.L.P. 3134, Postikodi 23106
Arusha-Tanzania

Uchapishaji na
Kitengo cha uchapishaji TANAPA
**Barua pepe:** cc@tanzaniaparks.go.tz

*Unaweza kupakua jarida letu hapa*

# YALIYOMO

4 Tahariri ya Mhariri

5 Ujumbe wa mhariri

6 Watoa maeneo yao bure kupisha barabara Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla

9 Mradi wa SOLA ulivyobadili maisha ya wavuvi Ziwa Tanganyika

10 Mtoto wa tembo awapigia 'saluti' wananchi waliomwokoa kisimani

14 Ufugaji nyuki chachu ya utunzaji mazingira Chato

18 Mgaraganza: Mfano wa kuigwa utekelezaji wa matumizi ya ardhi

20 Elimu ya uhifadhi shuleni yashika kasi

23 Burigi-Chato yagawa miche 16,000 ya miti vijiji vya Ngara, Chato

26 TANAPA yaipaisha shule Kigoma, kupandishwa hadhi

28 Miaka 50 ya KINAPA: Wadau waungana kupanda miti laki moja kila mwaka kuokoa barafu Mlima Kilimanjaro

31 Tanapa yawashika Mkono Chankele Ujenzi wa Shule

33 'Bila mchango wa TANAPA, Rubondo Sekondari isingekuwepo'

35 TANAPA yaadhimisha siku ya wanyamapori kwa kupanda miti

37 Mradi wa Ufugaji Nyuki Kufaidisha Vijiji vya Mwamgongo, Kiziba-Kigoma

# TAHARIRI YA MHARIRI



**Msomaji mpendwa**

**Mpendwa msomaji wetu wa Jarida la Ujirani Mwema, napenda kukualika tena kujisomea jarida letu pendwa. Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) limekuwa mstari wa mbele katika kusimamia na kuyahifadhi maeneo yaliyohifadhiwa hapa nchini yakiwa na hadhi ya hifadhi za Taifa.**

Usimamizi huu wa maeneo haya umekuwa ukienda bega kwa bega na ushirikishaji wa jamii inayozunguka hifadhi hizi kwani wananchi (jamii) ndio msingi mkuu katika uhifadhi wa rasilimali hizi. Kupitia mpango wa Ujirani Mwema wa TANAPA, wananchi wamekuwa wakipewa elimu, kushiriki katika shughuli mbalimbali za uhifadhi na kuwezesha miradi ya kijamii na ya kiuchumi ambayo huchungia utunzaji wa mazingira.

Kupitia jarida hili, utapata kujisomea na kujionea kazi mbalimbali zinazoendelea kufanywa na Shirika kupitia mpango wa Ujirani Mwema chini ya Kitengo cha Uhifadhi-Mahusiano ya Jamii. Kazi hizi zinajumuisha utoaji wa elimu kupitia njia mbalimbali ikiwemo kutumia walimu ili kuwafikia wanafunzi shuleni ambao ni kizazi cha kesho pamoja na ushiriki wa Shirika katika maadhimisho ya siku ya WANYAMAPORI duniani.

TANAPA inaendelea kutoa wito kwa jamii kuendelea kushiriki katika utunzaji wa mazingira na kuendelea kufichua vitendo vya uhalifu wa kuhujumu maliasili zetu. Katika kipindi cha mvua za masika, TANAPA inawaasa wananchi kushiriki katika upandaji wa miti ya asili na miti ya matunda ikiwa ni sehemu ya kutunza mazingira na kuendelea kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi yanayozidi kuonekana kila siku. Ni vyema pia tukaendelea kutumia nishati mbadala ambazo haziathiri mazingira yetu na kufanya shughuli za uzalishaji maji (shughuli za binadamu) ambazo hazileti madhara katika mazingira.

Uwepo wa migongano baina ya binadamu na wanyamapori umeonekana kuongezeka kila siku kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kupanuka kwa shughuli za kibinadamu kufuatia ongezeko la watu katika maeneo ambayo awali yalitumiwa na wanyamapori. TANAPA itaendelea kutoa elimu kwa jamii ya namna ya kukabiliana na wanyamapori hawa. Napenda kutoa rai kwa jamii kufanya shughuli ambazo hazikinzani na uhifadhi karibu na maeneo ya hifadhi kama vile uwekazaji wa mashamba ya wanyamapori, misitu ya hifadhi au ufugaji nyuki.

Aidha, maeneo ya mapito ya wanyamapori ni muhimu kwa ustawi wa wanyamapori kwa sababu huwezesha uwepo wa mwingiliano wa vinasaba na kuepusha kutoweka kwa spishi za wanyamapori kutokana na kukosekana kwa mwingiliano huo (inbreeding).

Nitumie fursa hii kukualika mpendwa msomaji wetu kuzitembelea hifadhi zetu za Taifa ili upate fursa ya kujivinjari pamoja na uwapendao. Hifadhi zetu zinafikika, na kuna shughuli mbalimbali ikiwemo kutazama wanyama kwa kutumia magari, utalii wa matembezi, kupanda milima, kupiga kasia, utalii wa puto na mengine mengi. Aidha, bei ni nafuu sana ukilinganisha na wageni ambao sio raia wa Afrika Mashariki.

Karibu uweze kujisomea na kufurahia makala zetu.

*Uhifadhi endelevu kwa maendeleo.*

William Simon Mwakilema
Kamishna wa Uhifadhi TANAPA

# UJUMBE WA MHARIRI



**Tunafurahi kukualika katika jarida letu pendwa la Ujirani Mwema upate fursa ya kujisomea kwa ajili ya kupata elimu na kupata taarifa juu ya shughuli mbalimbali ambazo zimetekelezwa na Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) katika jamii.**

Jarida hili linaendelea kutoa fursa kwa jamii na wadau wa uhifadhi kwa ujumla kupata taarifa kutoka uwandani na maarifa mbalimbali juu ya uhifadhi. Taarifa hizi zinaeleza kwa undani namna ambavyo TANAPA inaendelea kushirikisha jamii na wadau wengine katika uhifadhi wa rasilimali za asili tulizopewa na Mwenyezi Mungu.

Ni matarajio yetu kuwa, mpendwa msomaji utapata nafasi kubwa ya kujifunza, kuburudika na pia kupata taarifa mbalimbali zinazotokana na kazi zilizofanyika. Tunapenda kupokea maoni, ushauri na mapendekezo ili kuboresha jarida hili.

"Tumerithishwa Tuwarithishe".

Karibuni sana.



Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi, Dkt. Bakari Mnaya
Mkuu wa Kitengo cha Uhifadhi






# WATOA MAENEO YAO BURE KUPISHA BARABARA HIFADHI YA TAIFA MTO UGALLA

*Na Rukumbusia Musoma, Kaliua*

**Katika hali isiyo ya kawaida, wananchi wa kijiji cha Zugimlole kilichopo Wilaya ya Kaliua mkoani Tabora, wametoa sehemu ya mashamba yao kwa ajili ya barabara ya kufika Makao Makuu ya Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla, bila kudai fidia yoyote.**

Hatua hiyo ya kizalendo imetokana na utoaji elimu ya uhifadhi kwa wananchi hao ambao walihamasika na kuamua kutoa maeneo ya mashamba yao kupisha ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita 6.3 kutoka katika barabara kuu ya Kaliua-Mpanda.

Diwani wa Kata ya Zugimlole, Barikeka Ramadhani, anaeleza kuwa baada ya Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla kutangazwa rasmi 2019, wananchi walipewa elimu kwa kushirikiana na Mkuu wa Wilaya ya Kaliua na viongozi wengine.

"Wananchi walielezwa faida mbalimbali zinazoambatana na uwepo wa hifadhi, walihamasika na kwa kauli moja waliamua kutoa sehemu ya mashamba yao bila kudai fidia ili barabara ya kwenda makao makuu ya hifadhi ijengwe.

"Tulishirikiana na viongozi wa wilaya, wizara, kata na vijiji kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kuwa na hifadhi ya Taifa kama tunavyoona na kusoma kwenye historia juu ya hifadhi za Serengeti, Mikumi na Ngorongoro.

"Wenzetu wa TANAPA walikuwa wanalazimika kuzunguka umbali mrefu kwa ajili ya kufika katika eneo la ofisi (Iluma) kwa kuwa barabara waliyokuwa wanatumia ilikuwa mbovu, ndefu na yenye mbuga, kwa ujumla haikuwa nzuri sana kwa wenzetu," anasema Diwani huyo.





*Sehemu ya barabara ambayo wananchi walitoa maeneo yao kufika katika makao makuu ya Hifadhi*

Diwani Barikeka anasema kuwa, walilazimika kutoa elimu ya uhifadhi kutokana na eneo hilo kupandishwa hadhi kutoka pori la akiba na hifadhi ya msitu na kuwa hifadhi ya Taifa ambako shughuli za kibinadamu haziruhusiwi isipokuwa utalii na tafiti za kisayansi.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Zugimlole, Isaka Kasele, anasema alimuagiza Mwenyekiti wa kitongoji cha Iluma Ali Kamba, kupita na kuona uwezekano wa kuwa na barabara fupi ya kufika makao makuu ya hifadhi.

Anasema pia alimuagiza Mwenyekiti huyo atambue wamiliki wa maeneo ambayo barabara itapita na awaalike kushiriki kwenye kikao. Kupitia kikao hicho serikali ya kijiji iliwaelimisha kuhusu umuhimu wa barabara hiyo, nao wakawa tayari kutoa maeneo yao bila fidia yoyote.

“Tunashukuru wananchi waliitikia wito wa kuja kwenye kikao na baada ya kuwaeleza faida za hifadhi walitoa maeneo yao kwa nia moja kabisa bila kudai fedha yoyote,” anafafanua.

Alizidi kufafanua kuwa, kufuatia makubaliano yaliyofikiwa, waliandika muhtasari na barua kwenda Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla kuwaeleza utayari wao wa kutoa maeneo kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwenda hifadhini bila fidia.


Serikali ya kijiji iliona faida za kuwa na barabara hiyo ni pamoja na kujenga mahusiano mazuri na hifadhi, kupata urahisi wa kutalii hifadhini na uwezekano wa fursa za kiuchumi kuongezeka.



*Mhe. Barikeka Ramadhani, Diwani wa Kata ya Zugimlole akifurahi jambo katika kikao*

“Tulipotoa taarifa kwa uongozi wa hifadhi, walifika kukagua barabara pendekezwa, wakaona barabara hii itafaa zaidi kwa sababu ni fupi (kilomita 6.3) na yenye miinuko itakayohitaji madaraja machache ikilinganishwa na ya awali (Kilomita 9).

"Tulianza kwa kuweka alama za barabara na zilikaa kwa takribani mwezi mmoja na hakuna hata moja iliyotolewa kwa sababu wananchi walielewa, wakati wa kufyeka barabara wote walishiriki kikamilifu," alisema.



*Ramadhani Funulo mmoja wa watu waliotoa maeneo yao kupisha barabara*

Mhifadhi Mahusiano ya Jamii Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla, Sadick Mohamed, anaeleza kuwa wanashirikiana vyema na wananchi na wamekuwa wakiwaelimisha juu ya uhifadhi na utalii.

"Kwakweli wananchi wa Kijiji cha Zugimlole ni mfano wa kuigwa, siyo rahisi kwa wananchi kutoa maeneo yao kupisha ujenzi wa barabara bila kudai fidia.

"Ni dhahiri wameona umuhimu wa hifadhi na kwa kuona makao makuu ya hifadhi yanajengwa jirani na kijiji chao walihamasika.

"Sisi tunafarijika, tunaahidi kushirikiana na wananchi ili wawe mstari wa mbele kutumia fursa zinazotokana na uwepo wa hifadhi," alifafanua Mhifadhi Sadick.

Mheshimiwa Diwani anasema tayari wananchi wameona faida ya uwepo wa barabara.

"Kufuatia uwepo wa barabara hii, zipo faida ambazo tumezipata ikiwemo urahisi wa kusafiri na kusafirisha bidhaa na kuongezeka kwa thamani ya viwanja vilivyo pembezoni mwa barabara hiyo. Aidha, tumepokea wawekezaji watatu ambao wako tayari kuwekeza kwenye miundombinu ya utalii.

"Kuna kiwanja ambacho maeneo mengine kinapatikana kwa Sh. 60,000 ila hapa kinauzwa hadi Sh. 150,000," anaeleza Diwani huyo.

Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla ni miongoni mwa hifadhi sita mpya zilizoanzishwa hivi karibuni, nyingine ni Nyerere, Burigi-Chato, Ibanda-Kyerwa, Rumanyika-Karagwe na Kigosi.

Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla inatokana na kupandishwa hadhi sehemu ya Pori la Akiba la Ugalla lenye ukubwa wa kilomita za mraba 1,811 na Hifadhi ya Msitu wa Ugalla Kaskazini wenye ukubwa wa kilomita za mraba 2,054 na hivyo kufanya hifadhi hiyo kuwa na ukubwa wa kilomita za mraba 3,865.



# MRADI WA SOLA ULIVYOBADILI MAISHA YA WAVUVI ZIWA TANGANYIKA

## *Wasaidia kupunguza uchafuzi wa mazingira ziwani*

*Na Samwel Nassari, Kigoma*

**Kijiji cha Mtanga kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma ni miongoni mwa vijiji vya asili vilivyopo mwambao wa Ziwa Tanganyika vyenye wavuvi na wakulima vinavyopakana na Hifadhi ya Taifa Gombe.**

Kijiji hiki kiko kusini mwa hifadhi kikiwa na vitongoji sita ambavyo ni Mtanga A na B, Kazinga, Ngerwe, Kizuka na Mirumba. Kina kaya zipatazo 1,100 na wakazi 16,218 kwa mujibu wa sensa ya Taifa ya watu na makazi ya mwaka 2022.

Asilimia 90 ya wakazi wake hujishughulisha na uvuvi kama njia kuu ya uchumi wao na wachache hutegemea kilimo.

Kilimo kinachofanyika ni cha kujikimu kutokana na uwepo wa safu nyingi za milima na sehemu chache za tambarare kando ya ziwa ambazo hutumika kwa makazi. Kutokana na eneo kubwa la milima yenye miteremko mikali kutofaa kwa kilimo, limetengwa kuwa hifadhi ya misitu ya kijiji.

Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) kupitia Hifadhi ya Taifa Gombe limewezesha vikundi 10 vya wavuvi katika vijiji vya Mwamgongo na Mtanga kuanzisha mradi wa nishati ya jua (sola) katika shughuli za uvuvi. Mradi huo wenye thamani ya Sh. 171,660,000 unalenga kupunguza matumizi ya taa za chemli na mafuta ya taa yanayochangia kuchafua mazingira ya Ziwa Tanganyika.

Mradi umesaidia kuboresha mazingira ya uvuvi na kuongeza kipato kwa mvuvi mmoja mmoja, sambamba na kupunguza uchafuzi wa mazingira katika ziwa hilo lenye kina kirefu na maji baridi ambalo ni tegemeo kwa wakazi wa mwambao wa Ziwa Tanganyika katika nchi za Tanzania, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Zambia.

Mafuta ya taa ambayo awali yalitumiwa katika taa za chemli nyakati za kuvua samaki, huvuja ziwani na kuathiri viumbe hai, vipande vya chemli navyo huvunjika kutokana na upepo mkali ziwani na kuleta madhara kwa viumbe walioko ziwani.

Kwa mujibu wa baadhi ya wanufaika wa mradi huo, wanaeleza kuwa gharama za uvuvi kwa usiku mmoja zimepungua kutoka wastani wa Sh. 150,000 hadi Sh. 100,000.

Mtendaji wa Kijiji hicho, Hassan Malilo, anatoa ushuhuda wa manufaa ya mradi huo kwa wananchi wake na faida ya uwepo wa Hifadhi ya Taifa Gombe kwa kijiji hicho.

"Kupitia hifadhi, wananchi wamenufaika na mradi kwa kuwaongezea kipato lakini pia kijiji kimepata ufadhili wa kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi na kujengewa ofisi kupitia Taasisi ya Jane Goodall inayofanya utafiti wa sokwe-mtu katika hifadhi hiyo.



*Hassani Malilo, Mtendaji wa Kijiji cha Mtanga*

"Asilimia kubwa ya wananchi ni wavuvi ambao hutumia zana dhaifu. Tulipata elimu ya mazingira na tukaomba mradi ambao umesaidia kupunguza matumizi ya mafuta ya taa na hata pia kupunguza uchafuzi wa mazingira.

"Tunajivunia kuwa na jirani mwema anayechangia kutuinua kiuchumi," anasisitiza Mtendaji huyo wa Kijiji akiungwa mkono na wenzake.

Luchi Hamis, Hassani Rujana na Fatuma Maulid ni wanakikundi kutoka vikundi vya Umoja, Tupendane na Upendo vilivyonufaika na mradi huu.

Kwa nyakati tofauti wametoa ushuhuda kuonesha namna walivyonufaika na mradi huo.

Akiwa Baba wa familia yenye watoto saba na mmoja wa wanachama wa kikundi cha Umoja, Luchi Hamis, anakiri faida lukuki alizopata tangu walipoanza kutumia sola.

“Tangu tulipopata sola nne na betri zake mbili, tumepuguza matumizi ya kununua mafuta ya taa, kukodi betri pamoja na manufaa mengine.

“Kabla ya mradi tulikuwa tunatumia Sh. 150,000 hadi Sh. 180,000 kugharamia chakula, mafuta na kukodi betri kwa siku, na sasa tunatumia wastani wa Sh. 100,000 kwa siku.

“Kama kikundi tumefanikiwa kuanzisha kibanda cha biashara ya huduma ya fedha.

“Binafsi nimefanikiwa kuhudumia familia yangu, na sasa inauhakika wa kupata milo mitatu kwa siku, nimeboresha makazi kutoka nyumba ya nyasi na kuwa ya bati na ninasomesha watoto.

Kwa upande wake, Hassan Rujana, ambaye ni mwanakikundi cha Tupendane, anasema walipata sola mbili na betri moja.

Anaeleza mafanikio yake katika kipindi cha mwaka mmoja na nusu wa mradi kuwa ni pamoja na kuweza kununua mbuzi watano na ng’ombe wa maziwa.

“Nimenunua ng’ombe wa maziwa na mbuzi watatu ambao wamezaa na kufikia watano, isingekuwa huu mradi sidhani kama ningemudu. Pia nina uhakika wa kupeleka watoto shule,” anasimulia kwa kujiamini.

Halikadhalika, Fatuma Maulid kutoka kikundi cha Tupendane anaeleza kuwa pamoja na changamoto zilizojitokeza, kikundi kinaona manufaa ya mradi.

“Kikundi chetu kilipata sola mbili, na tumekuwa tukizitumia katika kazi zetu za kila siku na wakati mwingine tunazukodisha kwa wavuvi wageni kwa ajili ya kuchaji betri kwa gharama ya shilingi 3,000 kwa siku” alieleza Fatuma Maulid.

Uwezeshaji wa mradi huu umekuwa mfano wa kuigwa katika vijiji jirani vikiwemo Kigaliye, Kalalangabo, Kiziba na Bugamba.

Uvujishaji wa mafuta ya taa umepungua na Samaki hawana tena harufu ya mafuta hayo.

Mango Bakari ni Mkufunzi wa vikundi vya vikoba na katibu wa Chama cha Mapinduzi (CCM) katika kata ya Ziwani.

Anaeleza kuwa ameishi katika Kijiji cha Mtanga kwa muda mrefu na ameona mafanikio mengi yaliyotokana na uwepo wa hifadhi ya Gombe yakiwemo ujenzi wa miundombinu ya shule (vyoo na madarasa), miradi ya kuinua kipato na utoaji wa elimu ya uhifadhi.

“Ninaishukuru TANAPA kwani tumenufaika na tunajivunia ujirani mwema. Tumejengewa madarasa, matundu ya vyoo na kupewa samani kwa ajili ya wanafunzi na walimu wa shule za msingi Mtanga na Mara na Sekondari ya Kagongo. Tunaamini uwezeshwaji wa mradi wa sola hapa Kijiji cha Mtanga na ufugaji nyuki katika Kijiji cha Mgaraganza pia itasaidia kutunza mazingira.”

Aidha, TANAPA ilitoa kiasi cha Sh. 500,000 kwa mbegu (seed money) kwa kikundi cha COCOBA katika kijiji cha Mtanga ambacho kilitumika kukuza mtaji na kuhimiza biashara rafiki kwa mazingira.

Anatoa wito kwa jamii kushirikiana na hifadhi kuhakikisha wanakomesha vitendo vyote vya uhalifu na kutumia vyema elimu ya mazingira na uhifadhi wanayopatiwa ili iwasaidie.





# MTOTO WA TEMBO AWAPIGIA 'SALUTI' WANANCHI WALIOMWOKOA KISIMANI

*Na Rukumbusia Musoma, Kaliua*

**Katika maeneo mengi nchini, mnyamapori anaponasa kwenye matope au kutumbukia kisimani, nje ya hifadhi, ni nadra kuona wanakijiji wakimuokoa, badala yake humzunguka wakiwa na mikuki, mapanga na visu kwa ajili ya kumchinja ili wajipatie kitoweo.**

Haikuwa hivyo kwa wananchi wa Kijiji cha Zugimlole wilayani Kaliua, Mkoa wa Tabora, ambao waliamua kumnasua mtoto wa tembo baada ya kutumbukia kisimani na kukesha humo usiku kucha.

Mtoto huyo wa tembo alitumbukia katika kisima ambacho kilikuwa kimejaa maji ya mvua wakati yeye na kundi la tembo walipovamia eneo la makazi kusaka malisho.

"Nilipata taarifa juu ya mtoto wa tembo kutumbukia kisimani, nikamtafuta Mwenyekiti wa Kijiji, Isaka Kasele, ambaye aliwapigia simu Hifadhi ya Taifa Mto Ugala ambao tulikuja nao hadi kisimani kumuona mtoto wa tembo aliyetumbukia," anaeleza Ramadhani Kazyoba ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mazingira ya Kijiji cha Zugimlole.

Naye Mwenyekiti wa Kitongoji cha Iluma ambapo mtoto wa tembo alitumbukia kisimani, Ally Kamba, alisema ni kawaida kwa makundi ya tembo kwenda kijijini hapo usiku kula michikichi (miti ya mawese), na siku ya tukio la kutumbukia kisimani kwa mtoto wa tembo, haikuwa na tofauti.



*Mhe. Diwani Barikeka akionyesha Kisima ambacho mtoto tembo alidumbukia*

"Kama kawaida, makundi ya tembo yanapoingia kijijini tunajaribu kuwafukuza kwa njia tofauti na siku hiyo tuligongagonga mabanzi wakakimbia, baadaye tukamsikia mtoto wa tembo akilalamika," alisema Kamba na kuongeza:

"Baadhi ya wanakijiji waliokwenda kuchuma mboga jirani na kisima hicho alfajiri walimuona mtoto wa tembo akihangaika kujinasua kisimani.

"Wakaja nyumbani kuniambia na kama Mwenyekiti wa Kitongoji, nikaenda kushuhudia na kumkuta akihangaika. Alikuwa kinda tu, siyo mkubwa sana."

Mwenyekiti huyo wa Kitongoji aliondoka kwenda kumpa taarifa Mwenyekiti wa Kijiji Kasele ambaye alimpigia Mkuu wa Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla, akimtaarifu juu ya tukio hilo.

Anasema kuwa, watumishi wa Hifadhi hiyo walifika ofisi ya Kijiji cha Zugimlole na kisha kuelekea kisimani pamoja na viongozi wa kijiji na baadhi ya wananchi. Walimkuta mtoto wa tembo bado akihangaika kujinasua.

"Mkuu wa msafara kutoka hifadhini alinieleza nitafute vitendea kazi, hususan koleo na jembe. Nilipovileta tukaanza kuchimba upande mmoja wa kisima kwa kushirikiana na wahifadhi hadi tukamuokoa. Alitoka salama bila majeraha na baada ya kutoka alinyayua mkonga wake juu ikiwa ni kama saluti ya kutushukuru na kuaga kisha akatokomea zake porini," anaeleza Kamba.





*Wananchi wakichimba ili mtoto tembo aweze kuokolewa*

Kazyombo naye aliongeza: "Tulijadiliana na wahifadhi namna ya kumtoa tukakubaliana tukipanue kisima apate nafasi ya kutokea. Tulipomaliza alifanikiwa kutoka nje ya kisima, alisimama kwa muda mbele kidogo akitutazama kabla ya kupiga kelele na kutokomea hifadhini. Alikuwa hajaumia."

Akizungumza kwa niaba ya Hifadhi kuhusu tukio hili, Mkuu wa Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla Kamishina Msaidizi Lomi Ole Meikasi anawashukuru wananchi kwa ushirikiano walioonesha na utayari wao kwa ajili ya kuokoa maisha ya mtoto tembo.

"Wananchi wa Zugimlole mmekuwa mfano wa kuigwa kwa kitendo mlichokifanya leo. Hakika ile dhana ya tumerithishwa tuwarithishe hapa Zugimlole inafanya kazi kweli kweli, hakika tutafika mbali katika uhifadhi," alisema Mkuu wa hifadhi.

Diwani wa Kata ya Zugimlole, Barikeka Ramadhani, alisema tabia ya kupenda wanyamapori imetokana na juhudi kubwa za uongozi wa Wilaya ukishirikiana na uongozi wa kata, vijiji na vitongoji kutoa elimu katika vijiji vinavyozunguka Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla.

"Nawashukuru waliokuwa wakuu wa Wilaya ya Kaliua, Abel Msalama na Paul Chacha, kwa kushiriki kikamilifu kuhakikisha watu wanaozunguka hifadhi wanaelemishwa," alisema Barikeka na kueleza:



*Mhe. Ramadhani Barikeka akieleza jambo katika kikao katani Zugimlole*

"Tulielezwa wahifadhi ni majirani zetu wema na wajumbe katika Kamati ya Maendeleo ya Kata na serikali za vijiji wanavyopakana navyo. Aidha, hifadhi inaweza kusaidia shughuli za maendeleo ya vijiji Jirani kwa kuchangia asilimia 90 ya miradi ya maendeleo ikiwemo miundombinu ya elimu, maji, afya na barabara."

Hata hivyo, Diwani Barikeka anakiri kuwa kabla ya kupatiwa elimu, walizoea kuitumia hifadhi hiyo iliyokuwa chini ya Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), na Mamlaka ya Usimamizi Wanyamapori Tanzania (TAWA), kwa kilimo, uchungaji mifugo, ufugaji nyuki na matumizi mengine ingawa wahifadhi walikuwa wakiwakamata na kuwatoza faini.

"Mkoa wa Tabora tulizoea kuishi na TFS na TAWA, taasisi ambazo zilitujengea mazingira tofauti na TANAPA. Sasa hifadhi hairuhusiwi tena kutumika isipokuwa kwa shughuli za utalii wa upigaji picha, ni jambo jipya kwa jamii za ukanda huu. Tulizoea kusikia tu hifadhi za Taifa za Serengeti, Mikumi, Saanane na nyingine."

Alisema, mara baada ya eneo la hifadhi kukabidhiwa kusimamiwa na TANAPA, wahifadhi walitoa muda wa miezi sita kwa wananchi kukoma shughuli zao ndani ya hifadhi. Hatua hii ilifikiwa baada ya makubaliano kupitia mikutano na vikao mbalimbali vilivyojumuisha hifadhi, wilaya, kata na vijiji.

Mkuu wa Kitengo cha Mahusiano ya Jamii katika Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla, Mhifadhi Sadick Mohamed, alisema pamoja na wakazi wa vijiji vinavyozunguka hifadhi kuelimishwa, bado hifadhi inakabiliwa na changamoto ya ujangili na shughuli nyingine za binadamu.

"Hifadhi imejitahidi sana kufanya mikutano, semina na vikao vya uelimishaji kwa jamii inayoizunguka kwa lengo la kuwapa elimu ya uhifadhi. Baadhi ya maeneo tumeendelea kushuhudia vitendo hivyo ikiwa ni pamoja na kuingia usiku kulima na kulisha mifugo hifadhini," mhifadhi Sadick alisema.

Anatoa wito kwa jamii kuendelea kushiriki moja kwa moja kwenye uhifadhi ikiwa ni pamoja na kuwafichua wale wenye nia ovu dhidi ya rasilimali za hifadhi kwa ujumla.

Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla ilianzishwa mwaka 2019 baada ya kuunganisha maeneo mawili yanayojumuisha sehemu ya Pori la Akiba la Ugalla lenye ukubwa wa kilometa za mraba 1,811 na Hifadhi ya Msitu wa Ugalla Kaskazini yenye ukubwa wa kilometa za mraba 2,054.

Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla inapatikana katika wilaya za Kaliua na Urambo mkoani Tabora, ikizungukwa na kata sita na vijiji 19.

Umuhimu wa Hifadhi ya Mto Ugalla ni pamoja na kutunza uoto wa asili wa misitu ya miombo, kulinda maeneo maalumu ya kihistoria na kuhifadhi mfumo wa kiikolojia wa Ugalla-Moyowosi-Kigosi. Aidha ni sehemu muhimu ya makazi na mapito ya wanyamapori.



# UFUGAJI NYUKI CHACHU YA UTUNZAJI MAZINGIRA CHATO

***Na Mary Mtenga, Chato***




*Picha ya pamoja ya kikundi cha Mwambao Kikumbaitale Chato*

**Kikundi cha Mwambao kimekuwa mfano wa kuigwa wa kutunza mazingira ya kijiji na kurejesha uoto wa asili uliopotea kupitia mradi wake wa ufugaji nyuki.**

Kikundi cha Mwambao, kilianzishwa mwaka 2012 kijijini Kikumbaitale katika Wilaya ya Chato. Kilikuwa na wanachama 117 lakini sasa wamebaki 32, wanaume 18 na wanawake 14.

“Wenzetu walikosa subira, wakidhani wangetundika mizinga na kupata asali papohapo”, Mkufunzi wa vikundi vya ufugaji nyuki na Mwenyekiti wa Kikundi cha Mwambao, Paulo Charles, aliliambia *Ujirani Mwema* kjijini hapo hivi karibuni.

Alisema sababu nyingine ni takwa la kikundi kuwa na wanachama wasiozidi 35 kupata usajili ngazi ya wilaya ambalo lingewalazimu kutengeneza makundi yasiyopungua mawili.

Akieleza historia ya kikundi, Charles alisema baada ya yeye kupata mafunzo ya ufugaji nyuki CTC Ngara, alikutana na wadau waliomhamasisha wa shirika lisilo la kiserikali la CHEMA.

Aliporudi Kitumbaitale na kuwaeleza baadhi ya wanakijiji, walihamasika na kuamua kuunda kikundi cha ufugaji nyuki na serikali ya kijiji nayo ikabariki wazo hilo na kuwapatia eneo la kuanzisha mradi.

“Serikali ya kijiji ilitupatia eneo la mlimani la ekari 422 japo lilikuwa na vipara (bila ya

miti) kutokana na uharibifu uliofanyika wa kilimo, ukataji kuni na uchomaji mkaa ovyo," alisema Mwenyekiti wa kikundi.

Aliongeza kuwa ndani ya miaka minne ya awali, kikundi hakikuweza kufuga nyuki bali kilihakikisha kinalinda eneo lilotolewa ili kurejeresha uoto.

Kikundi kilianza kutundika mizinga eneo hilo mwaka 2016 kikianza na mizinga 54 ya kienyeji kabla ya shirika la CHEMA kukipatia mizinga 16 ya kisasa.

Kufuatia mafunzo waliyopewa ya aina ya mizinga bora na faida zake, kikundi kilitengeneza mizinga 12 ya kisasa mwaka 2017 na kufanya kiwe na jumla ya mizinga 28. Taratibu kiliachana na ile mizinga ya kienyeji inayotengenezwa kwa magome ya miti.

"Afisa Misitu na Meneja wa Wakala wa Misitu (TFS) Wilaya ya Chato walikuwa wakitutembelea mara kwa mara, pamoja na maafisa wa shirika la CHEMA, kuona maendeleo ya kikundi chetu.

"Mwaka 2018, tulifanikiwa kuvuna lita 60 za asali ambazo tuligawana wanakikundi kwa matumizi yetu wenyewe," alieleza Charles.



*Paul Charles, Mwenyekiti wa kikundi*

Mwaka 2019, kupitia ruzuku ya Mfuko wa Misitu Tanzania (TAFF), wanachama wawili walipewa mafunzo ya ufugaji nyuki na utengenezaji mizinga katika Chuo cha Misitu Tabora na kupata mizinga ya kisasa 254.

Kikundi kuliitundika mizinga hiyo msituni na kujenga mabanda mawili madogo (manzuki ya banda) yenye uwezo wa kuhifadhi mizinga 50 kila moja.



*Manzuki yenye mizinga 50 iliyotengenezwa kwa ufadhili wa Mfuko wa Misitu Tanzania (TAFF)*

Kwa kuwa kikundi kilikuwa bado kinahitaji mizinga na vifaa, kiliiomba Hifadhi ya Taifa Kisiwa cha Rubondo ikiwezeshe kupitia mpango wake wa Ujirani Mwema.

“Mwezi Oktoba 2022 hifadhi ilituchangia mizinga 125, vifaa vya kukamulia na kuchujia asali, jozi 20 za mavazi na vifaa vingine.

“Tumeshatundika mizinga 124, kati ya hiyo 47 ikiwa tayari na makundi ya nyuki porini,” alifafanua mwenyekiti wa kikundi.

Hata hivyo, alisema kipindi walichotundika mizinga hakikuwa na makundi mengi ya nyuki kwani kiliambatana na baridi na hakikuwa msimu wao kuingia kwenye mizinga. Wanatarajia mizinga mingi itapata nyuki baada ya kuvuna mwezi Juni mwaka huu 2023.

Mbali na kupata elimu ya mazingira na ufugaji nyuki, kuzalisha lita 609 za asali na kilo 75 za nta hadi mwaka 2022, mafanikio mengine ambayo kikundi kimeyapata ni pamoja na kutunza mazingira ya kijiji na msitu kulikopekea kuongeza mvua kijijini inayosaidia upatikanaji wa uhakika wa chakula miongoni mwa wanajamii.

“Aidha uyoga sasa unapatikana msituni na hivyo kuboresha lishe na kipato cha wanakijiji,” mwenyekiti huyo wa kikundi aliongeza.

Mtunza Hazina wa kikundi, Veronica Boniface, alieleza kuwa wamejiwekea utaratibu wa kugawa mapato yatokanayo na asali katika makundi manne ya asilimia 70 kwa ajili ya kukopeshana wanakikundi, asilimia 10 ya kuweka akiba benki, asilimia 15 ya kugawana kwa uwiano sawa miongoni mwa wanakikundi na asilimia 5 ya kutunza kwenye kikundi kwa ajili ya kuhudumia gharama za uendeshaji na dharura.

“Sisi hukutana kila tarehe 5 ya mwezi kuweka hisa za Sh. 1,000 za kutunisha mfuko. Fedha hizi pamoja na zile za asilimia 70 hukopeshwa kwa wananchama kwa shughuli zao za uzalishaji mali.

“Faida inayotokana na mikopo hugawanywa miongoni mwa wanakikundi kwa uwiano wa hisa, huku ile ya asilimia 15 ya mapato ya mazao ya nyuki hugawanywa kwa uwiano sawa pamoja na asali kidogo kwa ajili ya matumizi binafsi ya wanakikundi,” alieleza Veronica.

Wakieleza mafanikio binafsi waliyoyapata katika mradi wa ufagaji nyuki, baadhi ya wanakikundi walitoa ushuhuda wakisema wamepata mahitaji ya msingi ya familia zao yakiwemo kusomesha, kujipatia elimu na kupanua biashara.

Mwalimu Masumbuko Manyasi, mmoja wa wanachama walioonja matunda ya kikundi hicho cha ufugaji nyuki cha Mwambao, amepata elimu ya ufugaji nyuki, ameanzisha shamba lake la ufugaji na anasomesha watoto wake katika shule binafsi kutokana na asali anayonunua kwenye kikundi.

“Kupitia elimu niliyopata, nimefanikiwa kutengeneza na kutundika jumla ya mizinga 180 katika shamba langu na sasa mizinga 135 ina nyuki na mingine 60 iko kwa fundi kwa matengenezo.



*Veronica Boniface, Mtunza hazina wa kikundi*



*Mwalimu Masumbuko mmoja wa wanakikundi*

"Disemba 2022, nilirina lita 120 za asali," Manyasi alisema. Aliongeza kuwa amepeleka elimu ya ufugaji nyuki shuleni anakofundisha ambako kuna eneo kubwa linalofaa kwa ufuagaji nyuki.

"Nimeusihi uongozi wa shule utumie fursa hii na tayari kamati ya shule imekubali, mzinga mmoja umeshatengenezwa," Mwalimu Manyasi alilieleza *Ujirani Mwema.*

Naye Jaidina James, alieleza kuwa amewapatia watoto wake mahitaji ya shule, zikiwemo sare na madaftari kwa walioko shule ya msingi na sekondari, na ada na mahitaji mengine kwa mmoja aliyeko chuo.

Pamoja na kuwa nimebaki peke yangu kufuatia mzazi mwenzangu kufariki, mapato ya asali yamenisaidia sana," alikiri mwanakikundi Jaidina.

Desdeus Christopher naye amefanikiwa kununua cherehani inayomuwezesha kuendesha biashara yake ya ushonaji vizuri.

"Kupitia mikopo inayotolewa na kikundi, nimenunua cherehani na vitambaa ili kuwahudumia wateja wangu kwa wakati. Isingekuwa huu mradi, sidhani kama ningepiga hatua hii," Desdeus alisema.

Mwenyekiti wa kikundi alisema baada ya kuwa na mizinga zaidi ya 450 ya kisasa, wanatarajia kuvuna lita 6,000 za asali na kilo 300 za nta katika msimu wa Juni 2023.

Wameshafundishwa uvunaji wa mazao mengine ya nyuki yakiwemo maziwa na sumu ya nyuki ingawa wanashindwa kuyavuna kwa sasa kutokana na kukosa vifaa.

Kikundi kimekuwa kikiuza asali kwa kiasi cha Sh. 10,000 kwa lita, na Sh. 12,000 kwa kilo ya nta, kikitarajia kupata jumla ya Sh. milioni 60 kutokana na asali na Sh. milioni 3.6 kutokana na mauzo ya nta.

Kikundi kinakabiliana na baadhi ya changamoto zikiwemo za uelewa mdogo miongoni mwa wanajamii ambao huhujumu msitu kwa kukata miti, kuchoma moto, ukosefu wa baadhi ya vifaa muhimu vya kujikinga wakati wa kurina asali na mashine kubwa ya kukamulia asali.

Uwepo wa makundi machache ya nyuki kutokana na msitu kutokuwa mkubwa husababisha nyuki kuchukua muda mrefu kuingia kwenye mizinga.

Mhifadhi Greyson Chegere, Mkuu wa Kitengo cha Mahusiano ya Jamii katika Hifadhi ya Taifa Kisiwa cha Rubondo, alikiri kuwa kikundi cha Mwambao cha kijiji cha Kikumbaitale kimekuwa cha mfano wa kuigwa na vijiji jirani kwa utunzaji wa mazingira kutokana na faida zinazopatikana.

"Tulipokea maombi ya kikundi na kwa kweli tulifanikiwa kukiwezesha mizinga na vifaa vingine vilivyogharimu Sh. milioni 12.5.


"Shirika linaamini mradi huu utaleta mabadiliko chanya na chachu kwa jamii na utaongeza ushirikiano miongoni mwa wanajamii katika kufichua uhalifu na utunzaji wa mazingira," alisema Mhifadhi Chegere.

Mwenyekiti wa kikundi anaishukuru Serikali, Halmashauri ya Wilaya ya Chato, TFS, Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), SIDO na wadau wengine wa nyuki kwa michango yao mikubwa iliyowezesha mradi kupatikana na kufikia hatua iliyopo.

Charles alitoa wito kwa jamii kuhifadhi mazingira na kushirikiana bega kwa bega na Serikali na hifadhi kuhakikisha mazingira yanatunzwa.

Alisisitiza kuwa faida za kutunza mazingira ni pamoja na upatikanaji wa mvua za uhakika na usalama wa chakula huku akitolea mfano wa namna kijiji cha Kikumbaitale kinavyonufaika na uwepo wa misitu ya kijiji, Hifadhi ya Taifa Kisiwa cha Rubondo na ile ya Hifadhi ya Taifa Burigi-Chato.

# MGARAGANZA: MFANO WA KUIGWA UTEKELEZAJI WA MATUMIZI YA ARDHI




Kijiji cha Mgaraganza kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma vijijini ni moja ya vijiji vilivyofanikiwa kutekeleza mpango wa matumizi ya ardhi.

Kijiji hicho kimesajiliwa mwaka 1974 na kupimwa 1987, Mgaraganza ni miongoni mwa vijiji vinavyopakana na Hifadhi ya Taifa Gombe iliyoanzishwa mwaka 1968.

Kutokana na ongezeko la watu, kijiji cha Mgaraganza kina wakazi zaidi ya 14,000 ambao wanategemea ardhi iliyopo katika shughuli za kilimo cha zao la biashara (mchikichi) na mazao ya chakula.

Mpango wa matumizi ya ardhi ni jambo lisiloepukika kutokana na ongezeko la idadi ya watu katika vitongoji sita vinavyounda kijiji hicho ambavyo ni Kilembera, Kagina, Mlati, Katombo, Msela na Mgaraganza.

"Hapa ilipo ofisi ya kijiji katika kitongoji cha Mgaraganza, kuna watu zaidi ya 2,000, ardhi haiongezeki lakini watu wanaongezeka, hivyo inatulazimu kutafuta njia ya kukabiliana na changamoto hiyo," anafafanua Mwenyekiti wa Kijiji Said Wagala.

***Na Samwel Nassari, Kigoma***

**Mpango wa matumizi ya ardhi ni utaratibu ulioanzishwa nchini kuondoa migogoro ya matumizi ya ardhi katika maeneo mbalimbali.**

Unahusisha mgawanyo wa ardhi iliyopo ili kukidhi mahitaji ya wadau wote ya kilimo, ufugaji, utunzaji wa vyanzo vya maji, hifadhi ya misitu na mazingira kwa ujumla.

Ni utaratibu unaomwezesha kila mdau kutambua na kuheshimu mipaka yake, husimamiwa kwa kutumia sheria ndogo ndogo.



*Said Wagala, Mwenyekiji wa Kijiji cha Mgaraganza*

Anaeleza kuwa waliwasiliana na wadau mbalimbali na ndipo Taasisi ya Jane Goodall ambao ni wadau wakubwa wa uhifadhi katika Hifadhi ya Taifa Gombe walisaidia kupata suluhisho.

Wagala anafafanua kuwa, mwaka 2020 Taasisi ya Jane Goodall iliwezesha uandaji wa mpango wa matumizi ya ardhi kwa vijiji vinavyozunguka Hifadhi ya Taifa Gombe.

"Mpango tunaotumia ni wa miaka 10 kuanzia mwaka 2020 hadi mwaka 2030 ambao umeainisha matumizi ya makazi yenye ukubwa wa hekta 4,397.02 na hekta 34.46 kwa ajili ya huduma za jamii.

"Hekta 1,409.5 zimetengwa kwa ajili ya kilimo, hekta 358.79 misitu, hekta 212.82 hifadhi ya mito na hekta 2.45 ni maeneo ya viwanda," anafafanua Mwenyekiti huyo.

Katika utekelezaji wa mpango huo, Mwenyekiti anaeleza kuwa, mpango umesaidia kuondoa migogoro ya ardhi iliyokuwepo baina ya kijiji na hifadhi, kijiji na kijiji na miongoni mwa wananchi.

Aidha, anaeleza kuwa mpango umewezesha kulinda vyanzo vya maji na misitu, na kwa sasa kijiji kinapata mvua ya kutosha.

Anaongeza: "Kutokana na kukosekana kwa usimamizi wa sheria ndogo ndogo, wananchi wachache walifanya uharibifu na kusababisha mgao wa maji baada ya vyanzo vya maji kukauka lakini baadaye Serikali ya kijiji iliwaondoa wavamizi katika maeneo hayo na upatikanaji wa maji sasa umerejea katika hali ya awali."

Katika kukabiliana na uharibifu wa mazingira kijji kimeanzisha kitalu cha miti ambapo miche hupandwa kila mwaka na hivyo kijiji kuwa mfano kwa vijiji vingine.

Baadhi ya changamoto zilizopo katika utekelezaji wa mpango huo, kwa mujibu wa Wagala, ni pamoja na migongano ya kimaslahi miongoni mwa viongozi.

"Watu wanapotosha jamii kuhusu nia njema ya Serikali ya kijiji kutenga mita 500 za hifadhi kinga (buffer zone) kama eneo la msitu wa kijiji wakidai kuwa Serikali imeuza kwa hifadhi," anasisitiza Wagala.

Anataja faida wanazopata wanakijiji cha Mgaraganza kuwa ni pamoja na kupungua kwa migogoro ya ardhi, uhakika wa upatikanaji wa maji, mapato na matumizi sahihi ya rasilimali zilizopo na fursa ya kumiliki ardhi kisheria.

"Uwepo wa hati utasaidia wananchi kukopa na kufanya maendeleo zaidi," anasisitiza Mwenyekiti huyo.




*Ramani ya Kijiji cha Mgaraganza ikionyesha matumizi mbalimbali ya ardhi yaliyopo*

Mwenyekiti anakiri ushirikiano baina ya hifadhi na kijiji ni wa manufaa na wananchi wamepata miradi ya ujenzi wa miundombinu ya elimu (vyumba viwili vya madarasa, ofisi moja ya walimu na samani), ufugaji nyuki (mizinga 40) na elimu ya utawala bora na uhifadhi.

"Aidha, jirani zetu (Hifadhi ya Taifa Gombe) hushiriki kupambana na waharibifu wa msitu wa kijiji," Mwenyekiti anatanabahisha.

Mhifadhi Nelson Mcharo ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Mahusiano ya Jamii katika Hifadhi ya Taifa Gombe anaeleza kuwa kabla ya mpango wa matumizi ya ardhi, kilimo kilikuwa holela na miti kukatwa ovyo kwa ajili ya mkaa na mbao.

Aidha, anasema mabadiliko makubwa yameonekana kwa jamii kutokana na utayari wa kupokea elimu ya matumizi ya ardhi.

"Kijiji hiki ni cha mfano katika usimamizi wa mpango wa matumizi ya ardhi, viongozi wake wako mstari wa mbele kusimamia," Mhifadhi Mcharo anaeleza.

Mhifadhi anatoa wito kwa jamii kutunza na kusimamia mazingira na mpango wa matumizi ya ardhi ili kuondoa migogoro na kuwa na uzalishaji wenye tija.





# ELIMU YA UHIFADHI SHULENI YASHIKA KASI

*Na Mandela Kamuli na Greyson Chegere, Kagera*

**Mwaka 2021 Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) lilianzisha mpango wa utoaji elimu ya uhifadhi kwa kutumia walimu wa masomo ya Jiografia kwa kidato cha pili kwa shule za sekondari na Maarifa ya Jamii kwa darasa la tano katika shule za msingi.**

Mpango huo wa majaribio ulianza na hifadhi 10 ambazo ni Saadani, Mikumi, Udzungwa, Kitulo, Katavi, Gombe, Mahale, Kisiwa cha Rubondo, Ibanda-Kyerwa na Rumanyika-Karagwe.

Shule ya Sekondari Murongo na Shule ya Msingi Masheshe zilizopo wilayani Kyerwa ni miongoni mwa shule 34 (tisa za sekondari na 25 za msingi) zinazopakana na Hifadhi za Taifa za Ibanda-Kyerwa na Rumanyika-Karagwe ambazo ziko katika mpango huo.

Mwalimu Mlenge Kimawa, msadizi wa Mwalimu Mkuu na mwalimu wa somo la Mazingira Shule ya Msingi Masheshe, anaishukuru TANAPA kwa kuanzisha mpango huu, akieleza kuwa program ina maendeleo mazuri ikiwa ni pamoja na kuwafikia wanafunzi wengi.

"Tangu tuanze program mwaka 2021, tumewafikia wanafunzi 378. Tunaishukuru sana TANAPA kuona umuhimu wa kuanza kuwajengea watoto uelewa wa uhifadhi," Mwalimu Kimawa alisema.

Mwalimu huyo anaeleza kuwa wanafunzi wamejifunza umuhimu na faida za uhifadhi katika maeneo yao na wananchi wanapata elimu kupitia kwao.

"Tumefanikiwa kupanda zaidi ya miti 50 katika eneo la shule yetu, kutokana na hamasa ya elimu hii, mwaka huu tunatarajia kupanda zaidi ya miti 500, kutembea hifadhini kujifunza kwa vitendo na tuwe mfano katika utunzaji wa mazingira," alisema mwalimu huyo.



*Baadhi ya wanafunzi wa shule ya Msingi Masheshe iliyopo Wilayani Kyerwa wakiwa katika miti waliyopanda*

Juliana Ernest na Brea Robert ni miongoni mwa wanafunzi wa darasa la sita katika shule ya Msingi Masheshe waliopata elimu ya uhifadhi mwaka 2022, wanakiri kuwa elimu hiyo imewasaidia na wanatoa wito kwa jamii kuachana na vitendo vya ujangili na badala yake itunze hifadhi.

"Nimejifunza kuwa katika hifadhi za Taifa kuna baadhi ya shughuli haziruhusiwi kama vile kilimo, kuchunga mifugo na kuwinda. Aidha, kupitia elimu hii nimekuwa nikiwafundisha wazazi nyumbani na nimeotesha miti miwili shuleni na mmoja nyumbani," Juliana alieleza.

Naye Brea alieleza: "Kabla ya kupata elimu hii tulikuwa tukifanya uharibifu hifadhni ikiwa ni pamoja na kukata kuni na kupeleka mifugo ila sasa tumeacha. Ninatoa wito kwa jamii na wanafunzi wenzangu kuzipenda hifadhi na kutunza mazingira."

Mwalimu Isihaka Mimbi wa somo la Jiografia Kidato cha Kwanza na Elimu ya Uhifadhi katika Shule ya Sekondari Murongo alitanabaisha kuwa mwamko wa elimu ya uhifadhi kwa sasa unakua ukilinganisha na kipindi program ilipoanza ingawa bado wananchi wana uelewa mdogo juu ya hifadhi za Taifa kwa sababu ni kitu kigeni kwao.



*Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Murongo wilayani Kyerwa wakionesha igizo lililohusu uhifadhi wa maliasili*

"Tayari walioanza na program hii wameshamaliza kidato cha nne, na tunaona mabadiliko hata kwa wananchi. Tunaomba TANAPA waendelee kutoa elimu ya uhifadhi," anasema.

***...Idadi ya shule na walimu yaongezeka***

TANAPA imeendelea kupanua wigo wa utoaji elimu ya uhifadhi kwa kuongeza idadi ya shule na walimu wa masomo ya Jiografia kwa kidato cha pili na Maarifa ya Jamii kwa darasa la tano katika wilaya za Geita, Chato, Muleba, Sengerema na Kyerwa.

Jumla ya shule za msingi 32 na sekondari tatu zinazopakana na Hifadhi za Taifa Kisiwa cha Rubondo, Ibanda-Kyerwa na Rumanyika-Karagwe zilifikiwa na kufanya kuwa na Shule 77 kati yake 59 zikiwa za msingi na 18 za sekondari katika vijiji 52.



*Picha ya pamoja kati ya wahifadhi, walimu na mgeni rasmi (aliyekaa katikati) katika Hifadhi ya Taifa Ibanda-Kyerwa*

Akizingumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo, Katibu Tawala Wilaya ya Kyerwa Benjamini Mwakasyege, aliwataka walimu wakawe chachu katika ulinzi wa maliasili wakizingatia lengo la semina ni kuwajengea uwezo wa kutoa elimu ya uhifadhi ili wanafunzi na jamii kwa ujumla walinde hifadhi na maliasili zilizomo.

"...Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa hifadhi zinakuwa na ulinzi imara kupitia kamati za ulinzi na usalama za kata na wilaya. Elimu kupitia walimu itafanya uhifadhi uwe endelevu," alisema Katibu Tawala wa Wilaya ya Kyerwa Mwakasyege.

Mwalimu Mary Mwakyusa kutoka shule ya Msingi Bugonde anasema: "Mtoto anapopata elimu huwa haimtoki, ni balozi mzuri vile vile elimu inamjenga na atarithisha wengine."

Naye Mwalimu Johari Elias kutoka Shule ya Msingi Kibare anaishukuru TANAPA kwa kuwashirikisha walimu katika utoaji elimu ya uhifadhi shuleni kwani walimu ni kiungo muhimu katika jamii na wadau wa elimu.

"Tunaishukuru TANAPA kwa kutushirikisha katika mpango huu, ninaamini utafanikiwa na kuwafikia wananchi wengi. Walimu tuko tayari kutoa elimu hiyo katika mikutano mbalimbali ili kuwafikia wananchi," alisema Mwalimu Johari.

Wakuu wa Hifadhi za Taifa Ibanda-Kyerwa, Kisiwa cha Rubondo na Rumanyika-Karagwe waliwaasa walimu kutumia mafunzo waliyoyapata ili mpango huu uwe na tija katika ulinzi wa hifadhi na maliasili zilizoko.

"Nendeni mkawafundishe wanafunzi na jamii kwa ujumla waelewe kuhusu uhifadhi, waache mitazamo hasi kwani maeneo yaliyohifadhiwa ni muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu," alisema Mkuu wa Hifadhi ya Taifa Ibanda Kyerwa, Fredrick Mofulu.

Naye Mkuu wa Hifadhi ya Taifa Kisiwa cha Rubondo, Moronda Moronda, alisema: "Walimu wanakaa na wanafunzi kwa muda mrefu hivyo wasipoelimishwa kuhusu mabadiliko ya tabia nchi, wanaweza kuwa miongoni mwa majangili.

"Tunaamini program hii, itasaidia vizazi hadi vizazi na kupunguza ujangili," alisema Moronda.

Naye Mkuu wa Hifadhi ya Taifa Rumanyika-Karagwe, Charles Ng'endo, aliwaeleza walimu: "... tunatarajia mtakuwa mabalozi wa uhifadhi na mtawezesha malengo ya mpango huu yafikiwe, tekelezeni majukumu yenu ili kuzalisha mabalozi wengi zaidi," alisema Ng'endo.




# BURIGI-CHATO YAGAWA MICHE 16,000 YA MITI VIJIJI VYA NGARA, CHATO

***Na Leticia Magesa, Chato***

**Hifadhi ya Taifa Burigi-Chato imegawa miche ya miti 16,000 aina ya misonobari na mikaratusi kwa wakazi wa vijiji vitatu Wilayani Chato, Mkoa wa Geita, na Wilayani Ngara, Mkoani Kagera.**

Maamuzi ya kugawa miche hiyo yanatokana na mahitaji makubwa yaliyowasilishwa hifadhini kupitia Serikali za vijiji vya Kalebezo wilayani Chato, Mshikamano na Rwakalemela wilayani Ngara.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Kitengo cha Mahusiano ya Jamii katika Hifadhi ya Taifa Burigi–Chato, Mhifadhi Ombeni Hingi, anaeleza kuwa hatua hiyo imetokana na wananchi wanaozunguka hifadhi hiyo kukabiliwa na uhaba wa mazao ya misitu.





*Wananchi wakishirikiana na wahifadhi kushusha miche ya miti katika Kijiji cha Kalebezo wilayani Chato.*

Hali hiyo imesababisha wananchi hao kukosa nishati ya kupikia, mbao, fito na nguzo kwa ajili ya ujenzi.

Anasema upungufu wa mazao hayo, kwa kiwango kikubwa, umechangiwa na uvunaji holela na ukataji miti ovyo kwa kipindi kirefu bila kuwa na utamaduni wa kupanda miti mingine.

"Wananchi wanakiri kuwa hiyo ilikuwa sababu kubwa kwa baadhi yao kuingia hifadhini kutafuta kuni, mkaa, nguzo na mbao kinyume cha sheria".

"Baada ya kupata elimu ya uhifadhi, wameona umuhimu wa kupanda miti itakayowapatia mahitaji yao, kabla ya hapo hawakuwa na ujuzi wa kuotesha miche wala mahala pakupata mbegu kwani kijiji chao hakina wazalishaji wa miche," anafafanua Mhifadhi Hingi.



*Elimu ya Uhifadhi ikitolewa katika mkutano wa hadhara Kijiji cha Rwakalemela wilayani Ngara.*

Wananchi waliomba hifadhi iwape miche itakayowasaidia kupata mahitaji hayo badala ya kuyatafuta hifadhini kinyume cha sheria.

Hingi alisema, Hifadhi kwa kushirikiana na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) na wilaya za Chato na Biharamulo waligawa zaidi ya miche ya miti 16,000 kwa wananchi 55 walioomba kupitia serikali za vijiji.

Alifafanua kuwa wananchi 20 wa Kijiji cha Kalebezo walipata miche 8,000 (miche 4,000 kwa wananchi 18 wa Kijiji cha Mshikamano na miche 4,000 kwa wananchi 17 wa Kijiji cha Rwakalemela).

"Hifadhi iligawa miche kwa wananchi wa vijiji tajwa kwa kila mmoja kupanda shambani kwake," alisema Hingi na kuahidi kuwa hifadhi itaendelea kuwapa wananchi wote waliotayari.

Alisema, hifadhi pia itaendelea kutoa elimu ya uhifadhi juu ya umuhimu wa uhifadhi na utunzaji wa mazingira.

"Tutaendelea kuwaelimisha wananchi juu ya faida za hifadhi, wajibu wao katika kulinda maliasili pamoja na kudumisha mahusiano mema," Mhifadhi Hingi alisisitiza.

Mmoja wa wakazi wa Kijiji cha Kalebezo, Samuel Ngelela, alikiri kuwa wananchi wamehamasika baada ya kushuhudia baadhi yao wakivuna mbao na nguzo katika mashamba ya miti waliyopanda miaka michache iliyopita.



Mmoja wa wanufaika akionesha maendeleo ya miche aliyopewa

Mkazi mwingine wa kijiji hicho, Experansia Bonaventura, naye alikiri kuongezeka kwa ushirikiano baina yao na hifadhi tangu kuanzishwa kwake mwaka 2019.

Wananchi walishukuru hifadhi kwa kuendelea kutoa elimu ya uhifadhi na ugawaji miche na kuomba hifadhi kuchangia maendeleo ya vijiji katika nyanja za afya, elimu, maji na ujasiriamali.

Mhifadhi, Samwel Nassari, kutoka Makao Makuu TANAPA, aliwaeleza wananchi kuwa: "Mpango huo unatarajia kuwasaidia wananchi kupata mazao ya misitu mashambani mwao na kuongeza kipato kwa kuuza ziada ya mazao hayo.

"Ni matarajio ya TANAPA kuwa miti ya mikaratusi mtakayoanza kuvuna miaka mitano ijayo na misonobari miaka kumi na mbili itakua chachu katika utunzaji wa mazingira na ustawi wa maendeleo ya wananchi walio jirani na hifadhi," Nassari alisema.





# TANAPA YAIPAISHA SHULE KIGOMA, KUPANDISHWA HADHI

*Na Nelson Mcharo, Kigoma*

**Walimu wa Shule ya Sekondari Bitale iliyoko Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma wamelishukuru Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) kwa ushiriki wake kwenye ujenzi wa bweni na madarasa.**

Mkuu wa shule hiyo, Jeremiah Mgasa, amesema ujenzi wa bweni na madarasa wenye thamani ya Sh. milioni 169 umeiwezesha shule hiyo kuwa na matokeo mazuri ya mitihani ya kidato cha nne.

Amesema ujenzi wa bweni hilo na samani zake umewezesha watahiniwa kupiga kambi shuleni kabla ya mitihani ili kuwa karibu na walimu badala ya kurudi nyumbani.

Bweni lina uwezo wa kulaza wanafunzi 45 ambao wangelazimika kutembea umbali mrefu kutoka nyumbani kwenda shuleni na kurudi.



*Mwonekano wa bweni lilojengwa kwa ushirikiano kati ya TANAPA na wananchi wa Bitale*

Mgasa amesema changamoto zinazoambatana na kukosekana kwa bweni ni pamoja na wanafunzi kukosa mwamko wa elimu kutokana na vishawishi na kazi za nyumbani.

"Matokeo yameanza kuonekana ambapo baadhi ya wanafunzi wa kike walikuwa wakielekea kufeli lakini kutokana na uwepo wa kambi ya mitihani, kiwango cha ufaulu kimeongezeka," amesema Mgasa.

Akitoa mfano, Mgasa amesema mwaka 2021, kabla ya ujenzi wa bweni kukamilika, watahiniwa wa kike 44 kati ya 82 walifeli ikilinganishwa na mwaka 2022 ambapo wanafunzi nane waliofeli kati ya watahiniwa wa kike 54 hawakuwa kwenye kambi ya mitihani kutokana na wazazi wao ama kukataa au kutokuwa na uwezo wa kuchangia chakula.

Amesema mara nyingine walimu hulazimika kuchangia chakula cha kambi kwa wananfunzi wanaofanya vizuri kwenye masomo ambao wazazi wao hawana uwezo, akitoa mfano wa mwanafunzi mmoja ambaye alifaulu kujiunga na kidato cha tano.

Uwepo wa bweni lililojengwa kwa kushirikiana na TANAPA umeifanya Serikali kuongeza majengo mengine manne ambayo yapo katika hatua za mwisho za ujenzi. Ongezeko hilo la mabweni limesababisha shule hiyo kufikiriwa kupandishwa hadhi na kuwa na kidato cha tano pamoja na mchepuo wa elimu ya wenye mahitaji maalum.

"Ujenzi wa mabweni ukikamilika, watahiniwa wa kidato cha pili na cha nne watapiga kambi ya kudumu," amesema Mgasa.

Akiongelea kuhusu madarasa, mkuu wa shule amesema "upungufu wa madarasa sasa ni historia kutokana na ushiriki wa TANAPA kwenye ujenzi wa madarasa sita ambapo darasa moja linatumika kama maktaba."

Afisa Elimu Kata, Jafari Moshi, amesema wanafunzi wa kike watakuwa na mahudhurio mazuri iwapo shule zitakuwa na mabweni, kwani wengi wao wanalazimika kutembea umbali mrefu na wakati mwingine kufanya kazi ili wajiingizie kipato kwa ajili ya mahitaji yao ya msingi.

Akitolea mfano wa shule anazosimamia, amesema jumla ya wanafunzi 61 kati ya 468 waliochaguliwa kujiunga na masomo ya sekondari kutoka Bitale, Bubango na Kizenga waliacha shule mwaka huu.

"Mmoja wa wanafunzi walioacha shule amekutwa akifanya kazi za nyumbani," Moshi amesema.

Amewashutumu baadhi ya wazazi kwa kushindwa kutimiza wajibu wao na kuwalazimu wanafunzi wajitafutie vipato kwa ajili ya familia zao na hususan wazazi wa kike kuwaandaa mabinti kwa kuolewa badala ya kuzingatia masomo.

"Kaya nyingi za mwambao wa Ziwa Tanganyika zinaongozwa na wanawake ambao wameelemewa na mahitaji ya watoto," amebainisha Jafari Moshi.

## Elimu ya Uhifadhi

Mbali na mabweni na madarasa, Mwalimu Mkuu Mgasa amesema shule pia imenufaika na elimu ya uhifadhi kupitia mpango wa TANAPA wa kutumia walimu kutoa elimu hiyo kwa kidato cha pili katika somo la Jiografia.

Katika mpango huo, mkuu wa shule, mwalimu wa taaluma na mwalimu wa Jiografia walipewa mafunzo ya kutoa elimu ya uhifadhi shuleni.

"Wanafunzi wanapanda maua, wanachora ramani ya mfumo ikolojia wa Serengeti baada ya somo la uhamaji wa nyumbu, wanachora sokwe-mtu na wameomba itengenezwe sanamu ya sokwe katika lango kuu la kuingia shuleni," Mgasa amesema.



*Mwanafunzi wa shule ya Sekondari Bitale akitoa elimu ya uhifadhi kwa wenzake*

Aidha klabu ya mazingira ya *Roots and Shoots* iliyoanzishwa shuleni hapo imepanda miche ya miti ya mninga, matunda na kuanzisha kitalu cha miche ya miti.

Naye Afisa Elimu huyo wa Kata ya Bitale, Jafari Moshi, amelipongeza shirika la TANAPA kwa michango yake ikiwemo utoaji wa elimu ya uhifadhi ambayo imeboresha mazingira ya shule.

"Mazingira ya shule hii ya Bitale yanapendeza sana ukilinganisha na Kizenga na Bubango kwa kuwa wanafunzi wanatumia elimu ya uhifadhi kwa vitendo," Moshi amekiri.



# MIAKA 50 YA KINAPA: WADAU WAUNGANA KUPANDA MITI LAKI MOJA KILA MWAKA KUOKOA BARAFU MLIMA KILIMANJARO

*Na Zawadi Mahinda, Moshi*

**TAFITI zinaonesha kutoweka kwa barafu iliyo katika kilele cha Mlima Kilimanjaro ikiwa hatua madhubuti za kudhibiti mabadiliko ya tabia nchi hazitachukuliwa.**

Kwa mujibu wa tafiti hizo, tangu mwaka 1912 kumbukumbu za mlima huo zilipoanza kuhifadhiwa, barafu katika mlima huo imekua ikipungua kwa wastani wa nusu mita kila mwaka na kubashiri kuwa huenda ikaisha kabisa ifikapo mwaka 2050.

Pamoja na hatua mbalimbali kuchukuliwa, sasa wadau wa Utalii na Uhifadhi wamekubaliana kuanzisha kampeni kabambe ya kupanda miti 100,000 kila mwaka katika Mlima Kilimanjaro ikiwa ni sehemu ya kurudisha uoto wa asili wa mlima huo mrefu zaidi barani Afrika.

Kampeni hiyo kabambe ambayo imeanza msimu huu wa mvua pia ina lengo la kuhakikisha barafu iliyoko katika kilele cha mlima huo haitamalizika kutokana na mabadiliko ya tabia nchi yanayoathiri mazingira ya mlima huo.

Akitangaza kampeni hiyo katika maadhimisho ya miaka 50 tangu kuanzishwa kwa Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro (KINAPA) hivi karibuni, Kamishna wa Uhifadhi wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), William Mwakilema, alisema kampeni hiyo inahusisha wadau mbalimbali kuanzia ngazi ya chini.



*William S. Mwakilema, Kamishana wa Uhifadhi TANAPA*

Alisema kwa kuanzia, miti imepandwa katika Shule ya Msingi Samanga katika Wilaya ya Moshi Vijijini na katika Shule ya Msingi Useri iliyopo wilayani Rombo ikiongozwa na Mhe. Nurdin Babu Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro ikiwa ni sehemu ya kampeni inayoshirikisha wadau zaidi ya 700 wa utalii na uhifadhi.

"Kwa kupanda miti mingi katika maeneo yanayozunguka mlima, tunaamini kutarejesha unyevu unaohitajika kutunza barafu katika kilele cha mlima wetu na kwa kushirikiana na wadau wetu tuna uhakika wa kufikia malengo.

"Misitu inayozunguka mlima ikiwa katika urefu wa kuanzia mita 1,700 hadi 2,700 kutoka usawa wa bahari ina wanyamapori wengi na ikistawi vizuri itachangia jitihada za kupambana na mabadiliko ya tabia nchi na kurejesha uoto wa asili wa mlima ambao ni muhimu kwa barafu," alisisitiza Kamishna Mwakilema.

Akizungumza katika kilele cha kampeni hiyo, Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Mohamed Mchengerwa, alipongeza wadau kwa kuweka malengo ya kupanda miti 100,000 kila mwaka katika miteremko ya mlima huo na kwamba ni hatua muhimu na sahihi.

Alisema malengo hayo yanaenda sambamba na sera ya Taifa ya kupanda miti milioni tano ifikapo mwaka 2030 ikiwa ni mpango wa Taifa wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi ambayo athari zake zinaonekana waziwazi katika maeneo mengi nchini.

Aliwaonya baadhi ya wafugaji wanaoshiriki kuharibu mazingira kwa kuingiza mifugo katika maeneo yasiyoruhusiwa kisheria, zikiwemo hifadhi za Taifa, wakishirikiana na baadhi ya watendaji wa taasisi za uhifadhi wasio waadilifu waache tabia hiyo.

"Tunajua kuna baadhi ya wafugaji ambao wanawashawishi watendaji wa taasisi za uhifadhi ili waingize mifugo katika maeneo yasiyoruhusiwa hasa nyakati za kiangazi, tunawaonya waache mara moja," alisisitiza na kuongeza:

"Hatutasita kuchukua hatua kali za kisheria kwa wenye mifugo na wale watumishi wetu wachache wasio na maadili kwa kuhakikisha kuwa sheria inafuatwa kikamilifu na hakuna mfugaji anaingiza mifugo yake katika maeneo yasiyoruhusiwa kisheria."



*Mhe. Mohammed Mchengerwa (Mb)*
*Waziri wa Maliasili na Utalii*



*Wananchi Wilayani Longido walipokea miche ya miti kwa ajili ya kupanda katika maeneo yao*

Waziri huyo wa Maliasili na Utalii pia aliwataka wapanda mlima huo kuhakikisha wanatunza mazingira ya mlima kwa kuacha kutupa taka ovyo na kuitaka TANAPA kuweka miundombinu ya kukusanya takataka na mfumo wa ufuatiliaji.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini TANAPA, Mhe. Jenerali Mstaafu George Waitara, alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kumteua tena kuiongoza bodi hiyo kwa miaka mitatu mingine.

"Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu, kwa kuendelea kuniamini na ninapenda kumuahidi kwamba, kwa kushirikiana na wenzangu, tutahakikisha malengo mapana ya Shirika yanafikiwa kwa manufaa ya uhifadhi, utalii na nchi yetu kwa ujumla," alisisitiza Jenerali Mstaafu Waitara ambaye pia aliwahi kuwa Mkuu wa Majeshi.



*Maj. Gen (rtd) George Waitara, Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini TANAPA*

Maadhimisho ya miaka 50 tangu kuanzishwa kwa Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro (KINAPA) yaliambatana na shughuli za kusafisha njia za kupanda na kushuka watalii kutoka mlimani na midahalo ya kutunza mlima huo iliyohudhuriwa na wadau kutoka ndani na nje ya nchi.

Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro ni ya pili kwa kuingiza mapato mengi ya kigeni baada ya Hifadhi ya Taifa Serengeti na idadi ya watalii wanaotembelea hifadhi hiyo imeongezeka kwa asilimia 400 kutoka watalii 12,050 mwaka 2021 na kufikia watalii zaidi ya 47,000 hadi Februari 2023.

Kwa mujibu wa Mhe. Jenerali Mstaafu Waitara, ongezeko hilo limechangiwa na filamu maarufu ya "Tanzania: The Royal Tour" iliyotengenezwa chini ya muongoza watalii namba moja nchini, Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambayo imetumika kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo hapa nchini.



*Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi Angela F. Nyaki akihamasisha upandaji wa miti wakati wa kampeni ya uzinduzi wa kuotesha miti ndani ya Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro tarehe 9 Machi, 2023*



# TANAPA YAWASHIKA MKONO CHANKELE UJENZI WA SHULE

*Na Nelson Mcharo, Kigoma*

**Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) kupitia Mpango wa Ujirani Mwema limewezesha wananchi wa Kijiji cha Chankele katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma kupata manufaa yanayotokana na uhifadhi.**

TANAPA kupitia Hifadhi ya Taifa Gombe imeshirikiana na wananchi wa kijiji hicho katika ujenzi wa shule yenye madarasa matano na samani zake, ofisi moja ya walimu na jengo la choo lenye matundu 10.

Akizingumzia ushirikiano huo, Mwenyekiti wa Kijiji cha Chankele Iddi Buliba, anasema msongamano mkubwa wa wanafunzi katika shule ya msingi pekee kijijini hapo na wanafunzi kutembea umbali mrefu iliwalazimu kuanzisha shule mpya ya Mlama.

"Wanafunzi walikuwa wengi kwa shule moja kuhimili, na wengine walikua wakitembea umbali mrefu. Tuliomba jirani zetu Hifadhi ya Taifa Gombe na wakatusaidia kujenga shule ikiwa na madarasa matano, ofisi, vyoo na samani," alisema mwenyekiti wa kijiji.



*Iddi Bulimba, Mwenyekiti wa Kijiji cha Chankele*



*Majengo ya madarasa na ofisi ya walimu yaliyojengwa kwa ushirikinao kati ya TANAPA na wananchi wa Chankele*

Mwalimu Elisha Barkena, ambaye ni Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mlama, anaeleza kuwa shule ina wanafunzi 517, wasichana 240 na wavulana 277 ikiwa na darasa la awali hadi la saba.

Mwalimu Elisha, anaeleza kuwa shule hiyo imeshatoa wahitimu wa darasa la saba mara tatu huku idadi ya watahiniwa na ufaulu ikiongezeka.

"Mwaka 2020, watahiniwa 14 (49%) kati ya 29 walifaulu, mwaka 2021 waliofaulu ni 31(74%) kati ya watahiniwa 42 na mwaka 2022 wanafunzi 36 sawa na silimia 56 kati ya watahiniwa 66 walifaulu.

Anasema: "Kama wanafunzi wangeendelea kusongamana katika shule moja, isingekuwa rahisi kupata ufaulu huu," Alieleza zaidi mwalimu Elisha.

Mwalimu Elisha anaendelea kubainisha kuwa mbali na faida za kupata miundombinu ya elimu, wamenufaika na elimu ya uhifadhi ambayo hutolewa na Hifadhi ya Taifa Gombe na mwalimu wa somo la maarifa ya jamii darasa la tano aliyepata mafunzo ya elimu ya uhifadhi.

"Tumepata miundombinu ya shule na elimu ya uhifadhi ambayo imekuwa ikitolewa na afisa mahusiano wa Gombe. Aidha, wanafunzi wameanzisha klabu ya mazingira," aliezea zaidi Mwalimu Elisha.

Mwalimu Elisha anaeleza kuwa shule ina upungufu wa walimu wanne, madarasa sita, ofisi moja, nyumba 10 za walimu, matundu 13 ya choo na madawati 76.

Mwalimu Elisha anaeleza kuwa shule ina umeme wa TANESCO, wanaomba kuwezeshwa vifaa vya TEHAMA mfano kompyuta, mashine ya kupiga chapa (printa) na fotokopi.

Mkuu wa Hifadhi ya Taifa Gombe, Kamishna Yustin Njamas, anaeleza kuwa mradi huu umegharimu zaidi ya Sh. milioni 91 ikiwa ni mchango kutoka TANAPA huku wananchi wakichangia matofali, mchanga, mawe, maji na nguvu kazi.



# 'BILA MCHANGO WA TANAPA, RUBONDO SEKONDARI ISINGEKUWEPO'

*Na Greyson Chegere, Rubondo*

**Shule ya Sekondari Rubondo wilayani Chato imeliangukia Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) kufikiria kuchangia tena ujenzi wa madarasa mengine kutokana na shule hiyo kuzidiwa na ongezeko kubwa la wanafunzi.**

TANAPA ilishiriki kikamilifu kuianzisha shule hiyo ambayo ujenzi wake ulianza mwaka 2010 lakini ukakwama kutokana na michango ya wananchi kukatika ghafla.

Maombi ya vijiji vinne vya Kakanshe, Kikumbaitale, Butarama na Bukamila vya Kata ya Kigongo kwa Shirika kupitia Hifadhi ya Taifa Kisiwa cha Rubondo ya kumalizia ujenzi yalikubaliwa na kuiwezesha shule kuanza Kidato cha Kwanza mwaka 2019.

Shule hiyo iliyoanza na wanafunzi 138 sasa ina jumla ya wanafunzi 919 (wavulana wakiwa 506 na wasichana 404) wote wakitegemea madarasa 12 yaliyopo kwa sasa.

Mbali na ujenzi wa madarasa sita, viti 240 na meza 240 vilivyochangiwa na TANAPA, madarasa manne yalijengwa baadaye kwa nguvu za wananchi, ingawa baadhi hayajakamilika, na mawili yalijengwa kupitia mradi wa UVIKO-19.

Makamu Mkuu wa Shule ya Sekondari Rubondo, Geofrey Michael Malingumu anaeleza kuwa mwaka 2021, uongozi wa kijiji kwa kushirikiana na bodi ya shule ulianzisha ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa.

"Mwaka jana ujenzi wa msingi wa vyumba viwili vingine vya madarasa ulianza tena," anasema makamu mkuu huyo wa shule.

Hata hiyvo, ujenzi umeishia njiani kutokana na changamoto mbalimbali, ikiwemo wananchi kuhitajika kuchangia masuala mengine ya maendeleo ya kijiiji ikiwa ni pamoja na ujenzi wa ofisi ya kijiji na shule ya msingi.



*Muonekano wa madarasa yaliyojengwa kwa ushirikiano kati ya TANAPA na jamii*

Makamu mkuu huyo anasema, mradi wa UVIKO-19 nao uliongeza madarasa mawili, viti 100 na meza 100.

"Shukrani za pekee kwa TANAPA kupitia Hifadhi ya Taifa Kisiwa cha Rubondo kwa mchango wake mkubwa katika kuanzisha shule hii ambayo kufikia mwaka jana (2022) ilikuwa na Kidato cha Kwanza hadi cha Nne," anafafanua na kuongeza:

"Isingekuwa TANAPA kutushika mkono, huenda shule isingeanza kabisa nasi tusingekuwepo hapa."

Malingumu anasema mbali na vyumba vya madarasa, shule kwa sasa pia inakabiliana na changamoto za ukosefu wa madawati, mabweni - hasa kwa wanafunzi wa kike-maabara, ofisi na nyumba za walimu.

Walimu wanachangia ofisi moja na makamu mkuu wa shule na walimu wote wanaishi katika vijiji jirani na shule hiyo kwani hakuna nyumba ya mwalimu hata moja.

Pamoja na kuisaidia shule kwa mengi, Malingumu analiomba Shirika liifikirie tena shule hiyo kwani wastani wa wanafunzi zaidi ya 60 badala ya 40 wanalazimika kurundikana kwenye darasa moja.

"Wanafunzi wawili hutumia kiti kimoja na meza moja na baadhi yao huenda shule wakibeba stuli zao mikononi wakati wengine hukalia mbao zilizowekwa juu ya tofali darasani.

"Wanafunzi kulundikana madarasani huwa changamoto kwa walimu katika kusimamia mitihani hasa nyakati za mvua na jua kali kwani baadhi ya wanafunzi hufanyia mitihani darasani na wengine nje.

"Tunawatoa baadhi ya wanafunzi nje kuepuka kubanana na kuibiana majibu," anasema makamu mkuu huyo wa shule.

Akielezea changamoto ya shule kukosa mabweni, Malingumu anasema wanafunzi wa kike wanaotoka katika vijiji vya Butarama na Bukamila vyenye umbali wa takriban kilometa saba hadi kumi kutoka shuleni hulalamika kwa kukimbizwa na wavulana mapema asubuhi wanapowahi kwenda shuleni.

Anasema kutokana na changamoto ya umbali iliyosababisha baadhi ya wasichana kupata ujauzito na sababu nyingine mbalimbali za kifamilia, ukiwemo uchumi duni, kati ya wanafunzi 138 walioanza Kidato cha Kwanza mwaka 2019, waliomaliza Kidato cha Nne mwaka jana walikuwa 89.

"Mahudhurio ni mazuri, wachache tu ndiyo wenye utoro wa rejareja," anasema makamu mkuu wa shule akieleza moja ya sababu kuwa ni takwa la halmashauri ya wilaya na utawala wa mkoa kwa wanafunzi kupata chakula cha mchana.

"Tuliitisha kikao cha wazazi ambao wamekubaliana kuchangia debe moja la mahindi na kilo tano za maharagwe kila mmoja. Hata hivyo, asilimia zaidi ya kumi ya wazazi bado hawachangii kikamiifu," anaeleza.

Kamati ya wazazi ya shule hiyo iliamua kuwatenga nyakati za milo watoto wa wazazi wenzao 'wanaokaidi' kuchangia chakula na mboga.

Hata hivyo, mkuu wa shule aliongea na kila mzazi 'makaidi' kuepuka mtoto wake kupata madhara ya kiakili na kisaikolojia ambayo yangeweza pia kuathiri ufanisi wao masomoni. Pia walimu huzungumza na wazazi hao ili kuona namna ya kuwasaiidia watoto wao.

"Baadhi ya wazazi 'waliokaidi' walianza kupeleka mahindi na maharagwe shuleni kidogokidogo badala ya debe moja na kilo tano kila baada ya miezi mitatu kutokana na hali za wazazi kutofautina na matokeo yake yameanza kuonekana," anasisitiza Malingumu

Wilaya ya Chato ina shule za sekondari nne, mbili zikiwa zimeanzishwa ndani ya miaka miwili iliyopita.

Shule ya Sekondari Rubondo inaongoza katika kata ya Kigongo kwa ufaulu wa kati ya Daraja la I hadi la IV. Kwa matokeo ya mwaka jana, kwa mfano, hakuna aliyepata Daraja 0.

Malingumu anasema ushirikiano kati ya shule na Hifadhi ya Taifa Kisiwa cha Rubondo unazidi kukua na umewezesha wanafunzi kuwa na somo la uhifadhi.

"Hifadhi iliwapeleka walimu wawili kwenye mafunzo ya elimu ya uhifadhi ambao wanawahamasisha wanafunzi kuwa mabalozi wema wa uhifadhi kwa wazazi wao na jamii kwa ujumla ili wasijihusishe na uvuvi haramu.

"Kutokana na elimu ya uhifadhi, mazingira ya shule kwa sasa yamependezeshwa na miti na maua," anakiri makamu huyo wa mkuu wa shule.

Anasema shule ina walimu 10 wa kuajiriwa na Serikali na wanne walioajiriwa na wazazi kwa mujibu wa kikao chao rasmi na kufanya iwe na jumla ya walimu 14.

"Muhtasari wa kikao hicho ulipelekwa halmashauri ya wilaya," anaeleza, akisisitiza kuwa shule inahitaji walimu wengine wanane ili kukidhi mahitaji yake ya ufundishaji.

"Aidha, ingawa shule inafundisha somo la sayansi, ina chumba kimoja cha maabara bila vifaa vyake," anahitimisha makamu huyo wa mkuu wa Shule ya Sekondari Rubondo.



# TANAPA YAADHIMISHA SIKU YA WANYAMAPORI KWA KUPANDA MITI

***Na Samwel Nassari, Arusha***

**Katika kuadhimisha Siku ya Wanyamapori duniani mwaka huu, Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) limeshirikiana na wananchi wa Jiji la Arusha kupanda miti ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kupambana na mabadiliko ya tabia nchi.**

Maadhimisho ya siku hiyo ambayo yaliendana na kauli mbiu, *Uhifadhi Shirikishi,* huratibiwa na kutekelezwa na Sekretarieti ya Mkataba wa kimaTaifa wa kudhibiti biashara ya usafirishaji haramu wa viumbe ambao wako hatarini kutoweka duniani (CITES), ikishirikiana na wadau wengine.

Akizungumza wakati wa upandaji miti uliofanyika katika ofisi za Shirika za Njiro jijini humo, Kamishna wa Uhifadhi TANAPA alitoa wito kwa wananchi na wadau kuendelea kushirikiana na TANAPA kuhakikisha rasilimali za asili wakiwemo wanyamapori zinalindwa na kuhifadhiwa ili zisitoweke na vizazi vijavyo waweze kunufaika.

"Nawakumbusha wananchi kuwa wanyamapori hawajui mipaka hivyo pasipokuwa na ushirikiano wa dhati ni vigumu kufikia malengo ya uhifadhi.

"Wanyamapori hawatambui mipaka iliyoko kwenye makaratasi... ni jambo la msingi kushirikiana na wananchi kuhakikisha wanyamapori wako salama hata wanapotoka nje ya hifadhi. Pia tunawaelimisha wananchi wajilinde wao na mifugo yao isidhurike," alisisitiza Kamishna wa Uhifadhi TANAPA William Mwakilema na kuongeza:

"Wananchi wanauelewa mkubwa kuhusu uhifadhi jumuishi pengine zaidi ya wataalam wa wanyamapori, sisi tuko tayari pia kujifunza kutoka kwao," alisema.



*William Mwakilema, Kamishna wa Uhifadhi TANAPA*

Lengo la siku hii ni kujenga uelewa miongoni mwa wananchi juu ya umuhimu wa wanyamapori, utunzaji wa mazingira na kuzuia biashara haramu za spishi ambazo zinakaribia kutoweka duniani. Aidha, inalenga kuhimiza wananchi washiriki kuhifadhi maeneo ya wanyamapori.

Katika hatua nyingine alieleza kuhusiana na maadhimisho ya miaka 50 ya Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro na *CITES*.

“Mwaka huu 2023, maadhimisho ya siku ya wanyamapori duniani yanaenda sambamaba na kusherehekea mafanikio ya miaka 50 ya kuanzishwa CITES na KINAPA. Tunatambua mchango wa wadau katika uhifadhi, kwani peke yetu tusingeweza,” alisema Mwakilema.

Pamoja na kufanya ulinzi wa wanyamapori, Shirika limeona ni vema kupanda miti katika maeneo mbalimbali ili kuboresha hali ya hewa ambayo kwa kipindi cha hivi karibuni imekabiliwa na mabadiliko ya tabianchi.  Watumishi wa TANAPA walishiriki kikamilifu katika zoezi hilo.

Akimwakilisha Mkuu wa kitengo cha Uhifadhi Dkt. Bakari Mnaya, Mhifadhi Mary Mtenga anahimiza wananchi kujenga utamaduni wa kupanda miti na kuitunza.

“Tujenge utamaduni wa kupenda kupanda miti na kuitunza kwa ajili ya afya zetu. Sote tunapenda kupata kivuli na upepo mzuri ambapo ukiwa na miti unaweza kupata mvua, hewa safi na matunda” alisema Mhifadhi Mary.

Mmoja wa wananchi walioshiriki, Herman Lyimo, anaishukuru TANAPA kwa kuona umuhimu wa kuwashirikisha wananchi.

“Nawashukuru sana TANAPA kwa kutualika kushiriki kupanda miti, tumejisikia furaha na faraja kwa namna tunavyothaminika. Tuko tayari kushirikiana nanyi kulinda hifadhi zetu kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo,” alieleza Lyimo.












# MRADI WA UFUGAJI NYUKI KUFAIDISHA VIJIJI VYA MWAMGONGO, KIZIBA-KIGOMA

*Na Edmund Salaho*

**Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), limekabidhi vifaa kwa ajili ya mradi wa ufugaji nyuki vyenye thamani ya Sh. milioni 31 kwa vikundi vitatu vyenye wanachama 73.**

Akisoma taarifa ya utekelezaji wa mradi huo, Mkuu wa Hifadhi ya Taifa Gombe, Yustin Njamasi, alivitaja vijiji vya Mwamgongo na Kiziba kunufaika na mradi huo.

"Mradi huu uliibuliwa na wananchi ukilenga kutunza misitu ya kijiji inayopakana na Hifadhi ya Taifa Gombe pamoja na kuwapatia kipato. Mradi ulihusisha utoaji wa semina na ugawaji wa vifaa ikiwemo mizinga 160, mashine nne, jozi 16 za mavazi pamoja na vitoa moshi vinne," anasema mkuu wa hifadhi.




*Mhifadhi Wilison Maanga (wanne kulia) kwa niaba ya TANAPA akikabidhi mradi kwa Mkuu wa Wilaya ya Kigoma Mhe. Salum Kalli*

Aidha, Kamishna Njamasi, alibainisha kuwa shughuli za ujirani mwema zimekuwa zikifanyika tangu mwaka 1992 kwa ushirikiano kati ya hifadhi na vijiji jirani.

Akikabidhi mradi huo kwa wanakikundi, Mkuu wa Wilaya ya Kigoma, Salum Kalli, aliwaasa wananchi kushirikiana na hifadhi katika kutunza rasilimali hizi kwa faida ya sasa na ya baadaye.

"Niwatake wananchi kushirikiana na hifadhi katika ulinzi wa misitu, vyanzo vya maji na wanyamapori wakiwemo Sokwe-mtu. Aidha, mtunze mradi huu kwa faida za kiuchumi na kimazingira," alisema Kalli.




*Mhe. Salum Kalli (wa kwanza kulia) Mkuu wa Wilaya ya Kigoma akikabidhi mizinga wa wanakikundi*

Mkuu wa wilaya, alitoa rai kwa wananchi kujenga tabia ya kuzitembelea hifadhi za Taifa ili kujionea vivutio lukuki vilivyomo na kuchangia pato la Taifa.

Mbali na mradi huo, TANAPA imetekeleza miradi ya nishati ya umeme wa jua na miundombinu kama vile ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu ambayo imegharimu zaidi ya shilingi milioni 230 katika Kata ya Mwamgongo.

# RAMANI YA TANZANIA INAYOONESHA MAENEO YA HIFADHI ZA TAIFA




| Hifadhi | Ukubwa (Km²) | Mwaka ilipoanzishwa |
|---|---|---|
| Serengeti | 14,763 | 1951 GN 12 |
| Ziwa Manyara | 648.7 | 1960 GN 505,2009 GN 105 |
| Arusha | 552 | 1960 GN 237,2005 GN 280 |
| Ruaha | 20,300 | 1964 GN 464,2008 GN 28 |
| Mikumi | 3230 | 1964 GN 465 |
| Gombe | 71 | 1968 GN 234,2013 GN 228 |
| Tarangire | 2,600 | 1970 GN 160 |
| Kilimanjaro | 1,668 | 1974, GN 56,2005 GN 258 |
| Katavi | 4,471 | 1974 GN 1 |
| Kisiwa cha Rubondo | 457 | 1977 GN 21 |
| Milima ya Mahale | 1,577 | 1985 GN 262 |
| Milima ya Udzungwa | 1,990 | 1992 GN 39 |
| Saadani | 1,100 | 2005 GN 281 |
| Kitulo | 431 | 2005 GN 279 |
| Mkomanzi | 3,245 | 2008 GN 27 |
| Kisiwa cha Saanane | 3 | 2013 GN 227 |
| Burigi-Chato | 4,707 | 2019 GN 508 |
| Ibanda-Kyerwa | 299 | 2019 GN 509 |
| Rumanyika-Karagwe | 247 | 2019 GN 510 |
| Nyerere | 30,893 | 2019 GN 923 |
| Kigosi | 7,460 | 2019 GN 924 |
| Mto Ugalla | 3,865 | 2019 GN 936 |



# HIFADHI ZA TAIFA TANZANIA
## KITENGO CHA MAHUSIANO YA JAMII

ISO 9001:2015 CERTIFIED

# WAJUE WANYAMAPORI HATARI NA WAHARIBIFU KWA MUJIBU WA SHERIA



### SABABU ZA MIGONGANO

- Kupungua kwa maeneo ya wanyamapori
- Ongezeko la shughuli za binadamu karibu na maeneo yaliyohifadhiwa
- Mabadiliko ya tabianchi
- Kufungwa au kuzibwa kwa mapito ya wanyamapori maeneo ya mtawanyiko
- Ukosefu wa mipango na usimamizi wa matumizi ya ardhi
- Ukosefu wa elimu ya uhifadhi

### ATHARI ZINAZOTOKANA NA MIGOGANO YA WANYAMA PORI

- Uharibifu wa mazao ya wananchi
- Majeraha au kifo kwa binadamu
- Kujeruhiwa au kuuawa kwa mifugo
- Kuuawa au kujeruhiwa kwa wanyamapori kwa lengo la kulipiza kisasi

### TAHADHARI NA MAMBO YA KUZINGATIWA NA WANANCHI DHIDI YA WANYAMAPORI WAKALI NA WAHARIBIFU

- Kutoa taarifa za mapema kwa taasisi husika Namba za bure kwa TANAPA ni **0800110098** au **0734986517, 0734 986 518** au **080 011 0068, 0800110046 na 0800110059** au **0734986520**
- Epuka kukabiliana na wanyamapori bila mafunzo na vitendea kazi
- Kutofanya shughuli za kibinadamu karibu na maeneo yaliyohifadhiwa, shoroba na maeneo ya mtawanyiko
- Kuepuka kuoga kwenye maeneo ya maji (mito na maziwa) yenye mamba na viboko
- Kupanda mazao yasiyopendwa na wanyamapori
- Kutumia njia rahisi zisizo na madhara za kupambana na wanyamapori wakali na waharibifu

*"Uhifadhi Endelevu kwa Maendeleo"* ***TUMERITHISHWA TUWARITHISHE***

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

HIFADHI ZA Taifa TANZANIA

# ELIMU YA UHIFADHI WA MALIASILI



Hifadhi za Taifa Tanzania
Kitengo cha Uhifadhi Mahusiano ya Jamii,
TANAPA Makao Makuu,
Barabara ya Dodoma,
S.L.P. 3134, Postikodi 23106
Arusha-Tanzania

MITANDAO YA KIJAMII +255 747 426 310 tzparks tanzaniaparks Tanzania National Parks